JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
OFISI YA MKUU WA MKOA WA LINDI

# MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)









## TAARIFA YA MAFANIKIO YA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI MKOANI LINDI KUANZIA NOVEMBA 2013 HADI APRIL 2017


Imeandaliwa na;
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P. 1054
Lindi

## 1. UTANGULIZI

Muhtasari unaotolewa katika taarifa hii ni maelezo juu ya ushiriki wa Jamii ya Mkoa wa Lindi kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mchakato wa kutambua na kuandikisha kundi maalum la walengwa wa mpango wa taifa wa kunusuru kaya maskini. Muhtasari huu unahusisha shughuli zote zilizotekelezwa kuanzia mwanzo wa mradi mwezi Novemba 2013 hadi Aprili 2017. Aidha Muhtasari huu utaangazia mafanikio katika maeneo makuu manne ya mradi ambayo ni Uhawilishaji fedha (CCT), Ajira za muda (PWP), Uboreshaji wa miundombinu (TI) pamoja na Mpango wa Kuweka akiba na kukuza uchumi (LI). Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji na namna zilivyoshughulikiwa pia zimeelezwa katika taarifa ya makala hii. Kwa ujumla wake mpango huu ndio unajulikana kama TASAF awamu ya tatu (TASAF – III)

Mpango huu umelenga kutoa ruzuku ya fedha taslimu kwa walengwa kwa wakati, uwazi na uhakika kila baada ya miezi miwili. Mpango huu ni mwendelezo wa mpango wa TASAF awamu ya tatu (TASAF – III) baada ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupata mafanikio katika awamu mbili za TASAF. Aidha gharama za mpango huu zinachangiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Benki ya Dunia ulioanza mwaka 2013 na kutarajiwa kudumu kwa miaka mitano nchini.

Mpango una tumia utaratibu wa kijamii wa wananchi kujiletea maendeleo yao wenyewe kwa njia ya ushiriki na uwajibikaji wa Mamlaka za Vijiji/Mitaa na wanajamii katika utekelezaji.

Jambo la kukumbukwa ni kwamba pamoja na mahitaji mengine ya jamii hususani, zahanati/hospitali, shule, maji ya bomba, barabara nk. Binadamu yeyote sharti ashibe kwanza kwa ajili ya kumuwezesha kuwa na afya bora ya kuendelea kutumia huduma hizo na kuzihudumia ili kuwa endelevu. Kwa hakika mtoto mwenye njaa hawezi kwenda shuleni na kufuatilia msomo yake kwa ufasaha. Vilevile mama mwenye njaa na afya duni hawezi kujifungua mtoto mwenye afya njema na pengine mtoto anaweza kuzaliwa akiwa mfu au mama kupoteza maisha wakati wa kujifungua. Kwa upande mwingine hata wanaume watu wazima wenye njaa hawawezi kufanya kazi kwa tija na kuleta maendeleo katika jamii husika

Kwa hali hii maendeleo yanayotarajiwa na ambayo ni matumaini ya jamii ni ya watu na siyo ya vitu, hii ikiwa na maana kwamba mahali ambapo kuna miundo mbinu bora ya barabara, shule, zahanati n.k na wanajamii kushindwa kutumia huduma hizo kutokana na kutomudu gharama zake, hayana maana sana kwa jamii hiyo.

## 2. UTAMBUZI NA UANDIKISHAJI WA KAYA MASIKINI

Katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa Mkoani Lindi, mchakato wa utambuzi wa kaya maskini sana ulitambulishwa rasmi ukiwa na madhumuni ya kutambua kaya masikini na kupata taarifa halisi za wanakaya wote na vituo vya kutolea huduma za afya na shule watakayosoma watoto.

Zoezi la utambuzi wa kaya msikini sana lilianza mwezi Novemba 2013 ambapo timu ya wataalamu kutoka TASAF makao makuu ilifika katika maeneo ya utekelezaji ya Mkoa wa

Lindi kwa ajili ya kuwajengea uwezo waheshimiwa madiwani na uongozi wa Halmashauri (CMT) juu ya mpango wa Kunusuru kaya Masikini. Aidha timu ya wawezeshaji ngazi ya wilaya ilipatiwa mafunzo ya namna ya kutambua kaya masikini katika ngazi ya Kijiji. Kaya masikini zilichaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji/mtaa husika ambapo mwakilishi wa kaya kwa ajili ya kupokea malipo kwa niaba ya walengwa katika kaya alichaguliwa. Kaya yenye hali duni zilifafanuliwa kuwa ni zile ambazo zina sifa kama ifuatavyo;-

- Kaya inayoishi katika makazi duni na haiwezi kumudu milo mitatu kwa siku,
- Watoto ndani ya kaya wanasoma, hawajaandikishwa au wameacha shule kutokana na hali duni ya kaya,
- Watoto na wajawazito walio ndani ya kaya hiyo hawaendi vituo vya afya au zahanati kupata huduma za afya.

Wananchi walielimishwa juu ya malengo ya mpango, masharti ya mpango, anayotakiwa kutimiza mlengwa, faida za mpango, na hatua za awali zitakazomfanya kupata malipo ya kwanza.

Mwisho jamii ilishirikishwa katika kupitia na kupitisha orodha ya kaya maskini na kaya zilizo maskini zilizotoka kwenye mfumo wa komputa zilifanyiwa kazi ambapo zile kaya maskini sana ziliandikishwa kama walengwa wa Mpango. Mamlaka zote za Serikali za Mitaa/Halmashauri zilihusika kama maeneo ya utekelezaji katika Mpango wa **Kunusuru** Kaya maskini ambapo angalau 2/3 ya vijiji/mitaa vililengwa na kuhusishwa kulingana na kiwango cha umaskini na idadi ya watu.

Mara baada ya kukamilika kwa utambuzi wa kaya masikini, orodha ya kaya masikini iliandaliwa na kuidhinishwa na kupelekwa TASAF makao makuu kwa ajili ya kuingizwa kwenye mfumo wa kompyuta (PMT) kwa ajili ya kutoa orodha ya mwisho kwa ajili ya uandikishaji. Zoezi hili lilifanyika kwa awamu nne na lilidumu kwa muda wa wiki tano hadi Januari, 2014

Zoezi la uandikishaji wa kaya maskini lilianza rasmi mwezi Jauari, 2014 na kukamilika mwezi Februari, 2014 ambapo orodha ya mwisho ilipelekwa TASAF Makao makuu kwa ajili ya kuandaliwa malipo. Zoezi hili lilifanyika kwa awamu nne na lilidumu kwa muda wa wiki tano hadi Februari, 2014. Jedwali lifuatalo linaonyesha idadi ya kaya zilizotambuliwa na kuandikishwa kwa Mkoa wa Lindi.

| **Na.** | **Halmashauri** | **Idadi ya Kaya** | | **Idadi ya Vijiji** |
|---|---|---|---|---|
| | | Utambuzi | Uandikishaji | |
| **1** | Kilwa Dc | 5,933 | 5,923 | 58 |
| **2** | Liwale Dc | 3,097 | 3,094 | 46 |
| **3** | Lindi Dc | 9,741 | 9,734 | 88 |
| **4** | Lindi Mc | 2,762 | 2,754 | 30 |
| **5** | Nachingwea Dc | 5,867 | 5,865 | 69 |
| **6** | Ruangwa Dc | 6,890 | 6,871 | 52 |
| | **Jumla kwa Mkoa** | **34290** | **34241** | **343** |

## 3. UHAWILISHAJI FEDHA (CCT)

Malipo kwa kaya masikini sana yalianza mwezi Machi, 2014 kwa mara ya kwanza ambapo Halmashauri zote mkoani Lindi ziliweza kulipa ruzuku kwa walengwa wa mpango. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 walengwa wa mpango walikuwa wamelipwa ruzuku kwa awamu 19 mfululizo.

Ruzuku kwa kaya maskini zililipwa kwa kufuata vigezo vifuatavyo;-

- Kaya yenye mtoto mdogo chini ya miaka mitano anayetakiwa kutimiza masharti ya afya inastahili kulipwa Tsh 4,000.00 kwa mwezi.
- Kaya yenye mtoto wa kuanzia miaka 5 hadi 18 anayetakiwa kutimiza masharti ya elimu inastahili kulipwa Tsh 2,000.00 kwa mtoto kwa mwezi. Idadi ya juu ni hadi watoto wanne.
- Kaya yenye mtoto anayesoma kidato cha kwanza hadi cha nne inastahili kulipwa Tsh 4,000.00 kwa mtoto kwa mwezi. Idadi ya juu ni hadi watoto watatu
- Kaya yenye mtoto anayesoma kidato cha tano hadi cha sita inastahili kulipwa Tsh 4,000.00 kwa mtoto kwa mwezi. Idadi ya juu ni hadi watoto wawili.

Ruzuku hii hulipwa mara moja kwa kipindi cha miezi miwili. Hivyo kwa mwaka kaya huweza kulipwa kwa awmu sita.

Sifa kuu ya mchakato huu ni uhakika kwamba malipo yanapokelewa na walengwa waliokusudiwa kulingana na orodha ya malipo. Marejesho ya malipo yasiyopokelewa yanarudishwa benki kwa wakati muafaka. Aidha siri kuu ya mafanikio ya mchakato huu ni kuzingatia taratibu na muda ambavyo ni vitu vya msingi katika mchakato huu. Matokeo ya mwisho ya hatua za malipo ni kupokea ruzuku ya fedha taslimu kwa kila kaya lengwa. Mchakato unaishia pindi ripoti inapounganishwa na Mfumo wa TEHAMA (MIS).

Shughuli kuu katika mchakato huu ni kufanya malipo kila baada ya miezi miwili kuzifikia kaya za walengwa katika kila kijiji kulingana na utimizaji masharti. Vilevile kusimamia taratibu za kurejesha na kudhibiti malipo yasiyochukuliwa. Aidha maelekezo mahsusi ya hatua za malipo yaliyofanyiwa uhakiki na kulipwa upya kwa malipo ambayo hayakupokelewa katika kipindi cha miezi miwili iliyopita yalishatolewa kwa watendaji wote ili kuongeza umakini katika ulipaji wa fedha kwa walengwa.

Kupitia mpango huu kwa wastani jumla ya kaya 25,500 katika Vijiji 313 na Mitaa 30 Mkoani Lindi hupokea ruzuku za Kaya maskini kila baada ya miezi miwili tangu mpango huu uanze mwezi Machi 2014. Baadhi ya kaya hushindwa kupokea ruzuku wakati wa malipo kwa sababu mbalimbali ikiwemo kuhamia vijiji visivyo na mpango, kufariki au kukosa viogezo kwa kuwa Mjumbe wa serikali ya Kijiji. Fedha za walengwa hawa huwa zinarejeshwa Halmashauri na baadae kuwasilishwa TASAF makao makuu.

Zoezi la Malipo huambatana na zoezi la uboreshaji wa taarifa za walengwa kama ikitokea kaya imepata mtoto mchanga, mwana kaya kufariki au kuhama na maboresho mengine muhimu. Aidha, katika kipindi cha malipo ufuatiliaji wa fomu za utimizaji wa masharti ya afya na elimu hufanyika ambapo fomu huwasilishwa na Kamati ya Usimamizi (CMC) katika ofisi ya Mratibu wilayani na kuingizwa katika Mfumo wa MIS. Taarifa za malipo

huingizwa kwenye mfumo wa Opsys ili kuweza kutoa taarifa ya kiasi cha fedha kilichobaki wakati wa malipo na idadi ya kaya zilizolipwa na ambazo hazijalipwa.

**Mafanikio**

Mafanikio yanayoonekana kwa kaya hizi ni pamoja na;-

- Kaya kuweka akiba na kuanzisha miradi midogomidogo kama vile ufugaji wa kuku, ufugaji wa mbuzi na nguruwe na kuanzisha bustani za mboga mboga.
- Kuboresha makazi yao kwa kupaua nyumba ambazo zilikuwa na nyasi, kuweka simenti katika sakafu nk
- Kuimarika kwa uhakika wa chakula kwa kaya kuwa na uhakika wa kupata milo mitatu kwa siku tofauti na mlo mmoja hapo awali.
- Kuongezeka idadi ya wanakaya wanaojiunga na mfuko wa afya ya jamii (CHF)
- Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika ngazi ya vijiji kwa kuwa ruzuku husaidia katika kuongeza mzunguko wa fedha kwa wafanyabiashara vijijini.
- kuongezeka kwa mahudhururio ya wanafunzi katika shule za msingi na sekondari,
- Kuongezeka kwa usajili wa watoto katika shule za msingi
- Kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaohudhuria kliniki.




***Mlengwa akipokea ruzuku ya kaya maskini kwa kipindi cha mwezi Machi 2017 katika kijiji cha Mingoyo Manispaa ya Lindi, fedha hizi huwasaidia kujikimu kimaisha.***



***Moja ya Manufaa ya ruzuku kwa kaya maskini ni kuongezeka kwa mahudhurio na usajili wa wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari Mkoani Lindi. Pichani ni wanafunzi wa shule ya Msingi Mkupama Manispaa ya Lindi.***



***Ujenzi wa madarasa mawili shule ya Msingi Mkupama na matundu sita ya vyoo ukiwa umekamilika ikiwa ni pamoja na kuwekewa umeme wa TANESCO katika Manispaa ya Lindi. Kati ya matundu sita ya vyoo mawili ni***

***kwa ajili ya waalimu na manne ni kwa ajili ya wanafunzi. Jumla ya Wanafunzi 90 wanategemewa kunufaika na mradi huu.***



***Ruzuku ya Kaya maskini pamoja na ujira imeiwezesha kaya hii kujenga nyumba katika Kijiji cha Mkukwe wilayani Nachingwea.***





***Mlengwa kutoka katoka katika kijiji cha Dodoma wilayani Ruangwa amefanikiwa kujenga kwa ktumia fedha za ruzuku ya kaya masikini. Kushoto ni eneo ambalo nyumba yake iliangushwa na mvua na kulia ni nyumba aliyofanikiwa kujenga.***

## 4. UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU (TI)

Ni kawaida kwa jamii nyingi duniani kupima maendeleo ya mtu kutokana na hali ya umiliki wa vitu vya thamani hususani, nyumba, magari ya kifahari, nguo za kifahari, chakula kizuri, vyombo vya thamani vya nyumbani, samani za kisasa, vifaa vya muziki na mawasiliano n.k. Hata hivyo katika mazingira ya ukombozi wa jamii za kipato cha chini hususani katika nchi yetu ya Tanzania maendeleo yanayotakiwa na yanayosisitizwa ni hali ya jamii kubadilika kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine na ni lazima mabadiliko haya yawe ya kutoka katika hali duni ya maisha na kuwa na hali bora ya maisha.

Mfano jamii iliyokuwa haina kabisa huduma ya afya, elimu na maji safi ya kunywa majumbani au kuipata kutoka umbali mrefu kwa gharama kubwa, kupatiwa huduma hiyo katika mazingira yanayofikika na kwa gharama nafuu. Hii inaweza pia kuwa kwa huduma nyingine hususani miundombinu ya barabara, masoko, aidha mahali pengine jamii iliyokuwa na wanajamii wengi wanaokula mlo mmoja kwa siku kubadilika na kuwa na watu wengi au wote kula milo mitatu kwa siku.

Katika hukakikisha wanafunzi na watoto wa chini ya miaka mitano wanaotimiza masharti ya afya na elimu katika mkoa wa Lindi hawapati shida katika kutimiza masharti yao, TASAF makao makuu ilifanya tathmini ya upatikanaji wa huduma za elimu na afya katika mkoa wa Lindi mwezi Machi 2014. Vijiji vilivyoonekana kuwa na shida kubwa ya upatikanaji wa huduma hizi zilipewa kipaumbele katika awamu ya kwanza ya majaribio kama ifuatavyo;

| Na | Halmashauri | Idadi ya Miradi | Jina la Mradi/Miundombinu iliyoapatikana |
|---|---|---|---|
| **1** | Lindi Dc | 1 | Ujenzi wa madarasa mawili, Ofisi ya waalimu, Choo cha matundu sita, mfumo wa maji ya mvua na mfumo wa umeme jua katika S/M Linoha |
| **2** | Lindi Mc | 1 | Ujenzi wa madarasa mawili, Choo cha matundu sita, mfumo wa maji ya mvua na mfumo wa umeme katika S/M Mkupama |
| **3** | Nachingwea Dc | 1 | Ujenzi wa madarasa mawili, Choo cha matundu sita mfumo wa maji ya mvua na mfumo wa umeme katika S/M Joshoni |
| **4** | Ruangwa Dc | 1 | Ujenzi wa Zahanati, ununzi wa samani na vifaa tiba katika Kijiji cha Nankonjera |
| **5** | Liwale Dc | 1 | Ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Mbonde |
| **6** | Kilwa Dc | 1 | Ujenzi wa nyumba ya mganga katika Zahanati ya Miteja |
| | **Jumla kwa Mkoa** | **6** | |

Utekelezaji wa miradi hii ulianza katika vipindi tofauti kuanzia mwezi Julai 2015 hadi Desemba 2015 baada ya maandalizi kukamilika katika ngazi ya Halmashauri. Hadi wakati wa uandaji wa taarifa hii, miradi hiyo ipo katika hatua za kukamilishwa ili kuwezesha kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi katika Halmashauri zote Mkoani Lindi.

**Mafanikio**
Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya uboreshaji wa miundombinu kwa msimu wa mwaka 2015/2016 katika Mkoa wa Lindi ni pamoja na;

- Ujenzi wa Madarasa (yenye umeme) umekamilika katika vijiji vitatu vya Linoha, Joshoni na Mkupama na kutoa huduma kwa wanafunzi zaidi ya 230 waliokuwa wanakero ya uhaba wa madarasa.
- Ujenzi wa vyoo matundu sita maalamu kwa wanafunzi na walimu umeondoa kero iliyokuwepo awali ambapo walimu walikuwa wanachangia vyoo na wanafunzi katika shule za Linoha, Joshoni na Mkupama.
- Mfumo wa Maji uliojengwa katika madarasa umewezesha upatikanaji wa maji kwa muda wote katika shule za Linoha, Joshoni na Mkupama.

- Ujenzi wa zahanati wilayani Ruangwa na Liwale unatarajia kuondoa kero kubwa waliyokuwa wakiipata akina mama wajawazito wakati wa kujifungua ambapo iliwalazimu kusafiri umbali mrefu hadi hospital za wilaya ili kupata huduma hiyo.
- Kamati za usimamizi (CMC) zimejengewa uwezo katika masuala yahusuyo usimamizi wa miradi na baadhi wamepata ujuzi wa ujenzi.



***Choo cha kisasa chenye matundu sita kikiwa kimekamilika. Kati ya Matundu sita, mawili ni kwa ajili ya walimu.***

## 5. AJIRA ZA MUDA (PWP)

Halmashauri za Mkoa wa Lindi zimeanza rasmi utekelezaji wa Miradi ya ajira za muda mwezi Agosti, 2016 ambapo timu ya wataalamu kutoka TASAF makao Makuu iliwasili katika Halmashauri za Mkoa wa Lindi na kuwajengea uwezo timu ya uongozi ya wilaya (CMT) na timu ya wataalamu wa sekta za Mazingira, Misitu, Kilimo, Umwagiliaji, Maji na Idara nyingine zilizohusiana na miradi hii. Semina hii ilifuatiwa na uibuaji wa miradi 447 iliyoegemea katika utunzaji wa Mazingira kama vile upandaji wa miti, uanzishaji wa vitalu, uchimbaji wa malambo na ukarabati wa barabara.

Baada ya miradi kuibuliwa na kufanyiwa uchambuzi wa kitaalamu ili kujua thamani ya mradi, 25% ya gharama ya mradi inatumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na malighafi za mradi husika. Fedha hizi ni sharti ziombwe na kijiji/mtaa husika kutoka mamlaka ya utekelezaji/Halmashauri na kwa mujibu wa makubaliano na Benki ya Dunia utaratibu wa manunuzi ya vifaa na malighafi ni wa kutumia ushindanishaji wa nukuu ya bei kama ilivyo kwa miradi yote inaytekelezwa na kupata fedha kupitia program ya TASAF. Kwa mujibu wa mwongozo wa utekelezaji miradi ya ajira za muda, 75% ya gharama/thamani ya mradi ni malipo kwa walengwa (Ujira) walioshiriki katika ufanyaji kazi zilizoainishwa na kutekelezwa katika mpango wa ajira za muda kupitia mradi husika

Mara baada ya miradi kuibuliwa, utekelezaji rasmi wa miradi hii ulianza kwa vipindi tofauti tofauti kuanzia mwezi Desemba 2016 hadi Februari 2017. Zoezi hili linahusisha vijiji ya vilivyochaguliwa kwa ajili ya kunufaika na mpango mkoani Lindi. Walengwa wa mradi huu ni kaya maskini sana ambazo hupokea ruzuku ya kaya masikini. Kaya moja hulipwa kiasi cha Tsh 2300.00 kwa siku na kazi hufanyika kwa muda wa siku 15. Hivyo basi kaya huweza kulipwa ujira wa Tsh 34500.00 kwa siku 15. Miradi hii itatekelezwa katika vipindi vinne vya siku 15 kwa mwezi na hivyo kwa na siku 60 kwa mwaka.

| Na. | Halmashauri | Muda walioanza utekelezaji | Idadi ya miradi | Idadi ya washiriki waliolipwa Machi, 2017 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilwa Dc | Februari 2017 | 44 | 3814 |
| 2 | Liwale Dc | Machi 2017 | 46 | 2595 |
| 3 | Lindi Dc | Disemba 2016 | 223 | 9138 |
| 4 | Lindi Mc | Disemba 2016 | 65 | 2557 |
| 5 | Nachingwea Dc | Februari 2017 | 69 | 5600 |
| 6 | Ruangwa Dc | Hawatekelezi | | |
| | **Jumla kwa Mkoa** | | **447** | **23704** |

**Malengo ya mpango wa ajira za muda ni pamoja na**

- Kuziwezesha kaya masikini sana kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu hususani katika kipindi cha hari/muwambo
- Kuendeleza miundombinu/rasilimali itakayosaidia jamii nzima na
- Kuongeza ujuzi kwa walengwa wa mpango

Kama ilivyoelezwa hapo juu miradi hii iliibuliwa mwezi August 2016 kwa mbinu shirikishi za fursa na vikwazo katika maendeleo zinazolenga kuendeleza dhana ya matengamaji katika vijiji na mitaa. Timu ya wataalamu waliopata mafunzo kutoka kwenye kila Halmashauri ilisimamia zoezi hili katika ngazi ya Kijiji/Mtaa. Miradi iliyoibuliwa ni 447 ikiwa ni pamoja na Ujenzi/Ukarabati wa Mabwawa, Upandaji wa Miti, Ujenzi/Ukarabati wa Barabara na Udhibiti wa Maorongo.

Miradi hii inatumia teknolojia ya Nguvu kazi, hivyo zaidi ya asilimia 75 ya bajeti ya mradi ni stahili inayolipwa kama ujira kwa walengwa na asilimia isiyozidi 25 inatumika kwa ajili ya vitendea kazi. Kwa ujumla miradi hii inalenga katika kuhifadhi mazingira na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi.

Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2017 utekelezaji wa miradi ulikuwa umekamilika katika Halmashauri zote tano zinazotekeleza mpangu huu katika Mkoa wa Lindi. Baada ya kukamilika kwa siku 15, mahudhurio ya walengwa huletwa katika ofisi ya Mratibu wa TASAF wilaya kwa ajili ya maandalizi ya malipo. Maandalizi haya huchukua hadi wiki mbili kwa fedha (Ujira) kuwa tayari. Kwa sasa walengwa wameshalipwa ujira kwa Mwezi Disemba 2016 na wanaendelea kusubiria ujira wao kwa kazi walizofanya katika kipindi vilivyobakia.

**Mafanikio**

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya ajira za muda kwa msimu wa mwaka 2016/2017 katika Mkoa wa Lindi ni pamoja na;

- Jumla ya miradi 447 ya vitalu vya miche/Upandaji wa miti, Uchimbaji wa Malambo Ukarabati wa Barabara za jamii za pembezoni, Udhibiti/Ukarabati wa Makorongo iliibuliwa na kutekelezwa katika halmashauri tano zinazotekeleza mpango huu.
- Walengwa wapatao 23,704 walipatiwa ujira uliowawezesha kumudu gharama za maisha kwa vipindi tofauti kuanzia mwezi Desemba 2016 hadi Machi 2017.
- Vifaa vya utekelezaji vilinunuliwa ikiwa ni pamoja na Majembe (Ngwamba), Tolori, Chepe, Sululu, Visanduku vya huduma ya kwanza, Mabuti nk. Vifaa hivi vitatunzwa na kutumika tena katika msimu wa mwaka 2017/2018.
- Walengwa wamepata uzoefu juu ya upandaji miti, uchimbaji wa mabwawa na udhibiti wa Makorongo na hivyo kuhifadhi na kulinda mazingira.



***Muonekano wa bwawa linaloendelea kukarabatiwa na walengwa katika Kijiji cha Naipingo. Ukarabati unafanyika ili kuongeza kina cha bwawa ili kutunza maji mengi yatakayonufaisha wananchi wengi waishio katika Kijiji hicho.***



***Mkuu wa wilaya ya Nachingwea Bi Rukia Muwango (wapili kutoka kushoto) akikagua mradi wa ukarabati wa barabara ya Chiumbati Shuleni yenye urefu wa Kilomita 3. Kutoka kulia ni Mhandisi wa Ujenzi Ndugu John Masika, Afisa Ushauri na Ufuatiliaji Ndugu Elius Muyomba na baadhi ya viongozi wa serikali ya Kijiji.***



***Hapa Kazi tu! Haya yalikuwa ni maneno ya walengwa wa mpango kutoka kijiji cha Kilimarondo ambao wanashiriki katika mradi wa Ujenzi wa bwawa katika hatua za kujiongezea kipato ili kuondokana na umasikini. Bwawa hili lina ukubwa wa mita za ujazo 4662 na baada ya kukamilika litanufaisha zaidi ya kaya 300.***

## 6. KUWEKA AKIBA NA KUKUZA UCHUMI (LI)

Shughuli za uwekaji akiba na kukuza uchumi kwa kaya maskini sana zilianza mwezi Mei 2016 katika Halmashauri za wilaya ya Lindi na Manispaa ya Lindi na baadae kufuatiwa na wilaya za Kilwa, Nachingwea na Liwale mwezi March 2017. Wilaya ya Ruangwa haikuwepo katika mpango huu kwa kuwa ilikuwa haijaanza utekelezaji wa miradi ya ajira za muda.

Zoezi hili lilitanguliwa na mafunzo kwa wasimamizi wa mradi ngazi ya Kata kwa muda wa wiki moja ambapo baada ya mafunzo jumla ya vijiji vinne kwa kila Halmashauri za Mkoa wa Lindi ziliibua vikundi kulingana na idadi ya walengwa. Ilielekezwa kwamba vikundi viibuliwe katika idadi ya watu 10 hadi 15 kwa kikundi kimoja na kwamba utaratibu huu ni wa hiari. Halmashauri za wilaya ya Lindi na Manispaa ya Lindi zipo katika hatua ya kuweka akiba kwa kuwa wao walipata mafunzo na kuibua vikundi tokea mwaka 2016. Halmashauri za Kilwa, Nachingwea na Liwale zipo katika hatua ya awali ambapo mpaka sasa wanangojea kupata fedha za usimamizi ili waendelee na zoezi la kuibua vikundi zaidi.



***Washiriki kutoka Halmashauri ya Mji wa Masasi na Nachingwea katika mafunzo ya kuweka akiba na kukuza uchumi wakiwa katika mafunzo ambayo yalifanyika mwezi Machi 2017 katika ukumbi wa Halmashauri ya Nachingwea.***

## 7. CHANGAMOTO ZA JUMLA KATIKA UTEKELEZAJI TASAF – III MKOANI LINDI

Zifuatazo ni changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya uhawilishaji fedha, ajira za muda na uboreshaji wa miundombinu;-

- Mahitaji makubwa ya jamii maskini dhidi ya raslimali chache zilizopo serikalini kuwafikia wote kwa wakati mmoja na mwamko mdogo wa wananchi katika uchangiaji wa nguvu kazi wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

- Matumizi yasiyo sahihi ya pesa yanayofanywa na walengwa wa mpango pindi wanapopokea pesa zao (Ulevi kupita kiasi) na mahali pengine jamii bado haijaweza kutumia fedha wanazozipata kwa usahihi hasa juu ya kuweka akiba na kuanzisha ujasiriamali mdogomdogo.
- Kundi kubwa la wanaonufaika na mpango huu ni wazee hivyo kushindwa kufanya uwekezaji au uanzishaji wa ujasiriamali mdogomdogo kwa ajili ya maisha ya baadae.
- Dhana iliyojengeka miongoni mwa jamii kuwa serikali itatoa kila kitu kupitia miradi ya wafadhili.
- Uchache wa fedha za usimamizi zitolewazo na mpango wa TASAF – III kuweza kugharamia shughuli za uendeshaji katika Halmashauri na ngazi za msingi hususani Vijiji na Mitaa.
- Ucheleweshaji wa ujazaji wa fomu za mabadiliko ya taarifa za waliopoteza sifa toka vijijini, mfano; vifo vya walengwa ili kuwezesha malipo kulipwa kwa wanaostahili kwa wakati uliopangwa.
- Ufinyu wa raslimali fedha na rasilimali watu hususani watoa huduma za kitaalamu ngazi ya Kijiji (LSP) na wataalamu ngazi ya wilaya. Maeneo mengi LSP mmoja anasimamia vijiji viwili hadi vitatu ili kupunguza gharama za usimamizi.
- Kumekuwa na walengwa wazee ambao baadhi yao hawawezi kutembea na hawana watu wa kuwawakilisha katika kazi za miradi ya ajira za muda na hivyo kukosa ujira hizo kujiongezea kipato.
- Kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi hususani kwenye miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya ujenzi (TI) kama vile madarasa, zahanati, barabara n.k.
- Udanganyifu unaofanywa na baadhi ya watendaji na viongozi wa serikali za vijiji/mitaa na Kamati za usimamizi (CMC) juu ya walengwa waliopoteza sifa za kuendelea kupokea ruzuku za kaya maskini.

## 8. MBINU ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI MKOANI LINDI

Pamoja na changamoto zilizojitokeza mkoa umeendelea kushirikiana na Halmashauri kutatua changamoto hizo kwa kufanya yafuatayo:-

- Kushirikisha viongozi wa Vijiji na Mitaa katika kuhakikisha kuwa fedha zote zinazolipwa kwa walengwa zinatumika kwa ajili ya uboreshaji kipato cha kaya maskini na maisha katika jamii.
- Kushirikisha viongozi wa Vijiji na Mitaa katika kuhakikisha kuwa jamii inashiriki kikamilifu katika kuchangia nguvu kazi katika miradi ya maendeleo.
- Kutoa mafunzo ya rejea kwa watumishi ili waweze kuwa na uelewa wa kutosha wa ujazaji wa fomu za mabadiliko ya taarifa za walengwa ili kuwezesha malipo kulipwa kwa wanaostahili kwa wakati uliopangwa.
- Halmashauri za Wilaya na Manispaa zimekuwa zikitoa nyongeza ya fedha na vitendea kazi kugharamia shughuli za uendeshaji katika Halmashauri na ngazi za msingi pale upungufu unapojitokeza.
- Kufanya utaratibu ili kuwezesha walengwa ambao ni wazee sana waweze kufanya kazi katika maeneo wanayoishi na kujipatia ajira ya muda.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&